# KENYA NATIONAL EXAMINATION COUNCIL
# REVISION MOCK EXAMS 2016
## TOP NATIONAL SCHOOLS

**KAPSABET BOYS HIGH SCHOOL**
**KISWAHILI**
**KARATASI YA 2**
**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

**SCHOOLS NET KENYA**
Osiligi House, Opposite KCB, Ground Floor
Off Magadi Road, Ongata Rongai | Tel: 0711 88 22 27
E-mail:infosnkenya@gmail.com | Website: www.schoolsnetkenya.com

## KAPSABET BOYS HIGH SCHOOL KCSE TRIAL AND PRACTICE EXAM 2016

**102/2**

**Karatasi ya 2**

**Mwongozo wa kusahihisha**

1. **UFAHAMU MWONGOZO.**

**MASWALI**

(a) Eleza kilichosababisha kongamano la katiba la Lancaster (alama3)

- Waafrika hawakua wamehusushwa katika katiba ya mwaka wa 1920.
- Waafrika walitaka kuhusika katika masuala ya uongozi.
- Utetezi wa wanasiasa ulilazimu serikali ya uingereza kuitisha kongamano.

(b) Taja mambo matatu yaliyotiliwa-mkazo na raia katika maoni yao kuhusu katiba. (alama3)

- Utawala mwema na uwajibikaji wa viongozi.
- Kulinda haki za binadamu zikiwemo za wanawake, watoto na walemavu.
- Kanuni za usawa na ulinganifu.

(c) Eleza umuhimu wa katiba kwa mujibu wataarifa. (alama3)

- kuweka utaratibu na kanuni za utawala mf utawala wa kimikoa.
- Hufafanua vyombo vikuu vya serikali, mamlaka yavyo na mipaka yavyo ya kutenda.
- Hupambanua haki za raia.

(d) Taja sababu zilizochangia ubadilishaji wa katiba. (alama 3)

- Katiba iliyokuwa imeandikwa na watu wachache ilikuwa imefanyiwa marekebisho mengi.
- Viongozi na watu wenye uwezo na utajiri walipuuza katiba.
- Kutokana na uongozi uliokuweko wakati huo, watoto na watoto na walemavu walidhulumiwa na kukosa uwakilishi ufaao.

(e) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika taarifa. (alama 3)

- Kitovu : Chenye maana na umuhimu.
- Harakati : Shughuli za kufanya jambo fulani.
- Hamasisha : Kufanya jambo lieleweke na kukubalika.
-

**UFUPISHO**

2. Soma makala haya kisha ujibu maswali yanayofuata

(a) Thibitisha kuwa Kiswahili kimekuwa lugha ya kimaitaifa ( maneno 35 – 40( alama 7)

**Nakala Safi:**

- Kiswahili huzungumzwa na watu wa nchi mbalimbali mf Tanzania, Burundi, Kenya nk
- Hutumiwa katika visiwa vya sokta(Oman)
- Hutumika katika idhaa mbalimbali mf BBC
- Hufundishwa vyuo vikuu Afrika na hata Marekani, Japani. Zozote 2×3=6Alama 1mtiririko

b) Ukitumia maneno yako mwenyewe, eleza ujumbe ulioo katika aya ya mwisho.

- Wageni kutoka ng'ambo walikaribishwa vizuri.
- Wageni waliingiliana vyema na wenyeji.
- Wangozi waliitwa waswahili.
- Baadhi ya wenyeji walifunzwa kiislamu na biashara.
- Lugha ilienea kwa urahisi pamoja na sayansi.
- Kiswahili kilichukua msamiati wa kigeni kwa wingi.
- Pametokea dhana potovu kuwa lugha ya Kiswahili ni ya kigeni. Zozote 7×1=7.Alama 1 mtiririko.

**<u>SARUFI</u>**

1. Eleza sifa bainifu za saurit (j). (al 2)
   Kipauso
   Kaakaa gumu
   Ghuna
2. Tofautisha mofimu huru na tegemezi kwa kutolea mifano mwafaka. (al 2)
   Mofimu tegemezi – hutegemea mofimu nyinginezo ili kuleta maana
3. Unda neno lenye silabi ifuatayo KIKKIKI (al 1)
   Matwana
4. Tia shadda katika sentensi ifuatayo wachezaji wamo uwanjani. (al 1)
   Wacjezaji <u>wamo</u> uwanjani
5. (i) Kiimbo ni nini? (al 1)
   Ni kupanda na kushkuka kwa mawimbi ya sauti binadamu anapozungumza.
   (ii) Onyesha matumizi mawili ya kiimbo. (al 2)
   Taarifa – Mama amewasili
   Swali – Utasafiri lini?
6. Ainisha (al 3)
   Wasiorithishwa
   Wa – kiambishi cha nafsi ya tatu wingi
   si – kikanushi
   o – O' rejeshi
   rithi – Mzizi
   shw – kauti ya kutendeshwa
   a - kiishi
7. Sahihisha sentensi ifuatayo. (al 2)
   Sukari zilizowekwa mfukoni zimenyeshewa

   Sukari iliyowekwa mfukoni imenyeshewa
8. Eleza maana ya sentensi zifuatazo. (al 2)
   (i) Tunda lenyewe limeoza
   (ii) Tunda lenye shimo halinunuliki
   (i) Kusisitiza
   (ii) Umilikaji

9. Kanusha sentensi ifuarayo. (al 2)
   Ningalifuzu katika mtihani wangu ningali tuzwa.
   Nisingalifuzu katika mtihani wangu nisingalituzwa.
10. Tunga sentensi na ubainishe kilalizo. (al 2)
    Yeye ni <u>mkurungezi.</u>
11. Andika sentence usemi halisi.
    Rais alisema kuwa wangepata tiba ya bure kama bunge lingepitusha mswala huo.
    "Tutapata tiba ya burekama bunge litapitisha mswada huu," Rais alisema.
12. Tunga sentensi yenye muundo wa: (al 3)

Kiima, kiarifa, yambwa tendwa, yanbwa tendewa na yambua ala.
Mama alipika chakula ya mjomba kwa sufuria.

13. Changanua sentesi kwa kutumia jedwali. (al 4)
Wachezaji vikapu watakifanikiwa katika mechi hiyo watatuzwa medali

| S | | | | |
|---|---|---|---|---|
| KN | | | KT | |
| N | V | S | T | N |
| Wachezaji | vikapu | wakifanikiwa katika mechi hiyo | watatuzwa | medali |

14. Nyambua kitenzi hiki katika kauli iliyo mabanoni pa (tendeka) (al 1)
Peka
15. Bainisha virai katika sentensi hii. (al 3)
Juma alikwenda mjini kwa miguu
KN – Juma
KT – alikwenda mjini
Ke – kwa miguu
16. Tunga sentensi ludhihirisha matumizi mawili ya <u>KU</u>. (al 2)
Kiambishi kiwakilishi cha ngeli ya KU-KU <u>ku</u>cheka hu<u>kuku</u>napendeza
Kuanzisha vitenzi vya silabi moja kula, kuja
Kukanusha wakati uliopita si<u>ku</u>mwona
17. Onyesha matumizi mawili ya nukta mkato. (al 2)
Kutenganisha sentnsi mbili tulipowasili alikuwa sebuleni; alikota kutushughulikia
18. Toa maana mbili ya sentensi ifuatayo: (al 2)
Leleni!
(i) Amri
(ii) Wingi wa wahusika

**<u>ISIMUJAMII: (ALAMA 10</u>**

(a) (i) Eleza maana ya krioli. (alama 2)

- Ni pijini iliyoimarika na kuwa na watu wanayoizungumza kama lugha yao ya kwanz

(ii) Eleza sifa zozote tatu za krioli. (alama 3)

- Huwa na wenyeji kwa mfano; Krioli ya Haiti, Kridi ya Jamaica
- Huwa na miundo dhabiti ya kisarufi.
- Huwa na msamiati dhabiti unaoweza kutungiwa kamusi.
- Huwa na matumizi mapana katika Nyanja za siasa, muziki, vyombo vya habari na kadhalika.

(b) (i) Eleza maana ya Lingua Franka. (alama 2)

- Ni lugha inayotumiwa na watu walio na lugha tofauti kwa ajili ya mawasiliano kwa mfano Kiswahili katika eneo la Afrika Mashariki.

(ii) Tambua sifa zozote tatu za Lingua Franka. (alama 3)

- Huwa ni lugha ua mawasiliano kati ya watu wenye lugha zaidi ya moja.
- Yaweza kuwa lugha ya kwanza ya mzungumzaji au lugha ya pili na kwa watu wengine lugha ua kigeni
- Hukiuka mipaka ya kitamaduni
- Hukiuka mipaka ua kimaeneo - inaweza kutumiwa katika maeneo mapana.
- Hutumiwa na watu ambao lugha zao za mama ni tofauti